Mob. No. +255621132543
Email, rubanasec@gmail.com

RUBANA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 458,
BUNDA.

KUMB. NA. RSS /F. I /VOL. I /01 **11/12/2020**
JINA LA MWANAFUNZI_____
SHULE YA MSINGI _____
S.L.P _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUBANA, HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA, MKOA WA MARA MWAKA 2021.

1. **Utangulizi:**

Uongozi wa shule ya Sekondari **RUBANA** unayofuraha kukufahamisha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi imekuchagua kujiunga na masomo ya kidato cha Kwanza mwaka 2021, katika shule hii ya sekondari Rubana. Shule ya Sekondari Rubana ni Shule ya Serikali ya Kutwa. Ni shule ya mchanganyiko (Wavulana na Wasichana) iliyoko kusini mwa mji wa Bunda kando ya barabara kuu iendayo Mwanza, magharibi mwa mtaa wa Balili.

Masomo yote yatafundishwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili. Uwapo hapa shuleni mawasiliano yote hufanywa kwa kutumia Lugha ya Kiingereza.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza **tarehe 11/01/2021**, Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe 11/**01/2021** na mwisho wa kuripoti shuleni itakuwa ni tarehe **25/01/2021** ndani ya siku saba.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

A. Suruali mbili (02) za kitambaa cha rangi ya kaki (tetron) zenye marinda mawili upana wa chini 19-20 sm iwe na mkunjo wa nje (turn up)

Kwa waschana ni sketi mbili (02) za kitambaa cha kaki (tetron), rinda box ziwe ndefu zivuke goti.

Kwa wasichana na wavulana.

i. Viatu vya kamba rangi nyeusi vyenye visigino vifupi vya ngozi vya kufunika miguu na visipige kelele wakati wa kutembea kwenye sakafu.
ii. Shati mbili jozi (02) rangi nyeupe (mikono mifupi).
iii. Soksi nyeusi ndefu jozi mbili (2).
iv. Sweta moja (1) rangi ya damu yam zee ya kuvaa wakati wa baridi.
v. Tai rangi ya kaki urefu isivuke mkanda wa suruali au sketi upana Sm 7.5 na iwe na kibanio.

B. Rangi ya ijabu ifanae na sare ya shule.
C. Sare ya michezo
- Kwa wavulana ni T-shirt ya damu ya mzee, bukta ya bluu na raba ya michezo.

- Kwa wasichana T-shirt ya damu ya mzee, suruali ya trak sut ya blu na raba ya michezo.

Kumbuka miongoni mwa sababu zitakazo pelekea mwanao kutopokelewa ni pamoja na ushonaji was are usio zingatia maelezo.

2.2: MICHANGO.

Mzazi anatakiwa kulipia kiasi cha TSH. 8,500/= kwa muhula kwa ajili ya kuchangia walimu wa kujitolea "part time teachers" kwa ajili ya kupunguza uhaba wa walimu wa sayansi hapa shuleni.

Fedha zote zitalipwa benki **NMB** akaonti namba **30101600138 ELIMU YA KUJITEGEMEA . Kisha leta bank paying sleep.**

NB:
Hakikisha umelipa fedha hiyo mapema benki kabla ya kumleta mwanao kuripoti hatupokei fedha taslim.

2.3: MAHITAJI MENGINE.

i. Madaftari makubwa 9
ii. Begi la kubebea madaftari
iii. Kalamu za wino wa bluu au nyeusi za kutosha
iv. Mkebe wa Hisabati moja (1)
v. Dictionary 1 (English to English).
vi. Rula ndefu moja.

NB: Tafadhali sana siku ya kuripoti Shuleni fika na **Mahitaji** yako yote uliyoambiwa pamoja na **Sare za shule** zote ulizoambiwa ili usajiliwe.

3.0: SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

3.1: **Mambo muhimu ya kuzingatia uwapo shuleni.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na

h) Kutunza mali za umma.

3.2: Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa Mjamzito / kupata mimba.
i) Kuoa/ kuolewa
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
l) Kuwa na simu ya mkononi.
m) Kusuka nywele na kuwa na ndevu.

4.0: Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai shuleni.
c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

5.0: Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kwa ukamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

_____

YUSUPH KIBASO
MKUU WA SHULE.

Mob. No. +255621132543
Email, rubanasec@gmail.com

RUBANA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 458,
BUNDA.

HATI YA KUKUBALI KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021

Mimi **…….** (jina) nimepokea barua yako ya masharti ya kujiunga na shule ya sekondari Rubana.

Ninaahidi kutii amri zote halali zitakazotolewa na walimu na walezi wangu wengine shuleni. Nitafanya kazi zote zitakazoiletea shule yangu na Taifa langu sifa nzuri, maendeleo na heshima. Nitafanya jitihada katika masomo yangu wakati wote.

Naelewa kwamba wakati wote nitakapokuwa mwanafunzi sitaruhusiwa kufanya yafuatayo;

1. Kuvuta bangi au kutumia madawa yoyote ya kulevya.
2. kuoa au kuolewa.
3. kufanya mgomo.
4. kujiunga na makundi ya wahuni.
5. kufanya makosa ya jinai.
6. Kushiriki katika mapenzi

Sahihi ya mwanafunzi: …….

Anwani: ……..…….

……

UTHIBITISHO WA MZAZI

Nakubaliana na masharti ya shule kama yalivyotolewa hapo juu napia niko tayari kumuhudumia kwa mahitaji yote ya shule hadi atakapohitimu kidato cha Nne.

Jina la mzazi: ……..… Tarehe: …….…..

Mahali anapoishi mzazi …… Mtaa/Kijiji ……..

Kata ya …… Tarafa ya ……

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

To: THE MEDICAL OFFICER
……

……

FROM: HEADMASTER
RUBANA SECONDARY SCHOOL

RE: …… (Name of student)

Please examine the above named as to *his/her physical and mental fitness. The examination should include the following categories (I-III) each category or sub-category of which will render the application ineligible in case of a defect. (Pregnancy category IV) will also render a girl candidate ineligible for the school.

I. (a) eye-sight (b) Hearing (c) Limbs (d) speech
(e) Venereal disease (f) Leprosy (g) Epilepsy
II. Neurosis
III. Other serious disease
IV. Pregnancy

PART B: MEDICAL CERTIFICATE:
(To completed by a Government (Registered Medical Officer)

I have examined the above named and consider that *he/she is physically *fit/unfit and mentally *fit/unfit for full time secondary studies.

I. (a) Eye –sight_____
(b) Hearing _____
(c) Limbs_____
(d) Speech _____
(e) Venereal diseases _____
(f) Leprosy _____
(g) Epilepsy _____

II. Neurosis _____
III. Other serious disease _____
IV. Pregnancy _____

DATE: _____ SIGNATURE _____

STATION _____ DESIGNATION_____

***Delete as necessary**